

# تفسير آيات الصيام

*Tafsiri ya Aayah za Swaum*

*Mwandishi:*

ʿAllamah na Shaykh

Ahmad bin Yahyaa an-Najmiy

*Tarjama:*

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

ʿAishah ʿUthmaan Nuʿmaan

## YALIYOMO

Utangulizi.....	3
Aayah za swawm.....	5
Watu waliokuwa kabla yetu walikuwa wakifunga.....	7
Lengo la swawm ni kumcha Allaah.....	8
Funga ni idadi ya masiku yenye kuhesabika.....	9
Kufunga siku ya shaka.....	10
Mgonjwa na msafiri katika Ramadhaan.....	11
Uhalisia wa safari.....	12
Swawm ya asiyeweza.....	13
Qur-aan imeteremshwa katika Ramadhaan.....	15
Qur-aan ndio maisha ya watu.....	17
Mkazi ni lazima kwake kufunga.....	18
Wenye udhuru kulipa siku zilizowapita.....	19
Wepesi wa Allaah kwa Allaah.....	20
Idadi ya siku za Ramadhaan.....	21
Takbiyr katika usiku wa ʿIyd na mchana wake.....	22
Swalah ya ʿIyd.....	23
Allaah yuko karibu na waja wake.....	24
Hutopata mabadiliko katika desturi ya Allaah.....	25
Msamaha wa Allaah na ukarimu wake.....	27
Kuanza na kuisha kwa swawm.....	29
Iogopeni mipaka ya Allaah.....	31
Kuiadhimisha mipaka ya Allaah ni katika ʿibaadah kubwa.....	32

## UTANGULIZI

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Himdi zote anastahiki Allaah. Tunamhimidi Yeye na kumuomba msaada na msamaha. Tunajilinda Kwake kutokamana na shari ya nafsi zetu na uovu wa matendo yetu. Hakika yule aliyeongozwa na Allaah, basi hakuna wa kumpoteza, na yule aliyeptezwa na Allaah, basi hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah, hali ya kuwa peke yake hana mshirika, na nashuhudia ya kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake. Allaah amswalie yeye, kizazi chake na Maswahabah wake.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تَقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُوا إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ

"Enyi mlioamini! Mcheni Allaah kama apasavyo kuogopwa na wala msife isipokuwa nyinyi [mmeshakuwa] ni Waislamu." (03:102)

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا

"Enyi watu! Mcheni Mola wenu Ambaye Amekuumbeni kutokana na nafsi moja na Akaumba kutoka humo mke wake na Akaeneza kutoka hao wawili wanaume wengi na wanawake. Na mcheni Allaah Ambaye Kwake mnaombana na jamaa. Hakika Allaah Amekuwa juu yenu ni Mwenye kuchunga." (04:01)

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَمَنْ يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا

"Enyi mlaomini! Mcheni Allaah na semeni kauli ya kweli [ya sawasawa]. Atakutengenezeni ‘amali zenu na Kukusameheeni madhambi yenu; na anayemtii Allaah na Mtume Wake, basi kwa yakini amefanikiwa mafaniko adhimu." (33:70-71)

Hakika maneno ya kweli kabisa ni Kitabu cha Allaah na uongofu bora ni wa Muhammad (Swalla Allahu ‘alayhi wa sallam). Mambo maovu kabisa ni yale ya kuzua. Kwa kuwa kila kilichozuliwa ni Bid’ah na kila Bid’ah ni upotevu na kila upotevu ni Motoni.

Amma ba’d:

Nitazungumzia baadhi ya Aayah kutoka katika Suurah "al-Baqarah", nazo ni zile Aayah ambazo Allaah ametufaradhisia kupitia kwazo swawm na akataja baadhi ya hukumu zake. Ninamuomba Allaah kwa unyenyekevu ajaalie kazi hii iwe imefanywa kwa ajili Yake pekee na amnufaishe nayo na kumpa faida yule (Subhaanah) Anayemtaka.

Ee Allaah! Hakika mimi nakuomba msamaha kwa yale nisiyoyajua. Hakika Wewe unajua na mimi sijui. Hakika Wewe ndiye mjuzi wa yaliyofichikana. Ee Allaah! Nitunuku uwerevu na unilinde na shari ya nafsi yangu. Ee Allaah! Hakika mimi najitenga mbali kutokamana na nguvu na uwezo wa nafsi yangu na ninatambua nguvu na uwezo Wako.

## AAYAH ZA SWAWM

Allaah (‘Azza wa Jall) amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ أَيَّامًا مَّعْدُودَاتٍ ۗ فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۗ وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامُ مِسْكِينٍ ۗ فَمَن تَطَوَّعَ خَيْرًا فَهُوَ خَيْرٌ لَهُ ۗ وَأَن تَصُومُوا خَيْرٌ لَّكُمْ ۗ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ ۗ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ۗ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۗ يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ وَلِيُكْمِلُوا الْعِدَّةَ وَلِيُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَاكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۗ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۗ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ أُحِلَّ لَكُمْ لَيْلَةَ الصِّيَامِ الرَّفَثُ إِلَىٰ نِسَائِكُمْ ۗ هُنَّ لِيَنَاسٍ لَّكُمْ وَأَنتُمْ لِيَنَاسٍ هُنَّ ۗ عَلِمَ اللَّهُ أَنكُم كُنْتُمْ مَخْتَلَتُونَ أَنفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ وَعَفَا عَنكُمْ ۗ فَالآنَ بَاشِرُوهُنَّ وَابْتَغُوا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ ۗ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَيْثُ يَتَّبِعَنَّ لَكُمْ حَيْطُ الْأَبْيَضِ مِنَ الْحَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ ۗ ثُمَّ أَتُوا الصِّيَامَ إِلَى اللَّيْلِ ۗ وَلَا تُبَاشِرُوهُنَّ وَأَنتُمْ عَاكِفُونَ فِي الْمَسَاجِدِ ۗ تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَقْرُبُوهَا ۗ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لِّلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

"Enyi mlioamini! Mmefaradhishiwa kufunga kama ilivyofaradhishwa kwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Allaah. [Kufunga ni] siku za kuhesabika. Yule atakayekuwa mgonjwa miongoni mwenu au safarini, basi akamilishe idadi [ya siku zilizompita] katika siku nyinginezo na kwa wale wanaooweza lakini kwa tabu watoe fidia kulisha masikini. Na atakayejitolea kwa jema lolote lile basi ni bora kwake. Na mkifunga ni bora kwenu - mkiwa mnajua [namna ilivyo kheri kwenu]! Mwezi wa Ramadhaan ambao imeteremshwa humo Qur-aan ili iwe mwongozo kwa watu na hoja bayana za mwongozo na pambanuo la batili. Basi atakayeshuhudia miongoni mwenu mwezi mpya na afunge. Atakayekuwa mgonjwa au safarini basi atimize idadi katika siku nyinginezo. Allaah anakutakieni mepesi - na wala hakutakieni magumu. Na ili mkamilishe idadi [katika wakati wake uliyowekwa] na ili mumtukuze Allaah kwa kuwa amekuongozeni na ili mpate kushukuru. Na pindi watakapokuuliza waja Wangu kuhusu Mimi, basi Mimi ni Niko karibu; Naitikia du'aa ya muombaji anaponiomba. Basi waniitikie Mimi na waniamini Mimi ili wapate kuongoka. Mmehalalishiwa usiku wa kufunga swawm kuwaingilia wake zenu. Wao ni vazi kwenu na nyinyi ni vazi kwao. Allaah anajua kwamba mlikuwa mkizihini nafsi zenu. Kwa hivyo amekukubalieni tawbah yenu na akakusameheni. Basi sasa waingilieni na tafuteni aliyokuandikieni Allaah. Kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni swawm mpaka usiku. Na wala msichanganyike nao hali ya kuwa nyinyi ni wenye kukaa P'tikaaf misikitini. Hiyo ni mipaka ya Allaah, hivyo basi msikaribie. Hivyo ndivyo Allaah anavyobainisha Ayah Zake kwa watu ili wapate kumcha."<sup>1</sup>

<sup>1</sup> 02:183-187

Aayah hizi zina mambo mengi. Nimeandika nukta thelathini na mbili au thelathini na tatu juu yake. Kupitia kalima hii nitajitahidi kuzitaja kwa ufupi na kwa njia ya faida kwa yule msomaji.

## WATU WALIOKUWA KABLA YETU WALIKUWA WAKIFUNGA

Allaah (Ta'ala) amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ

"Enyi mlioamini! Mmefaradhishiwa kufunga kama ilivyofaradhishwa kwa waliokuwa kabla yenu."<sup>2</sup>

Hapa Allaah (‘Azza wa Jall) anatumbaridha kwamba ametufaradhishia na kutuwajibishia swawm kama alivyoiwajibisha kwa wale ambao walikuwa kabla yetu. Allaah aliwawajibishia wale ambao walikuwa kabla yetu kufunga siku tatu kila mwezi na siku ya ‘Aashuura’. Imesemekana vilevile kuwa Allaah aliwawajibishia wana wa Israa’iyl kufunga Ramadhān. Halafu wakaongeza siku kumi na hapo ndipo swawm ikawa siku arubaini. Kisha mmoja katika wafalme wao akawa mgonjwa ambapo akawa ameweka nadhiri kuongeza siku kumi endapo atapona. Kitu ambacho alikifanya. Wakawa wanafunga siku khamsini. Ni jambo lisilokuwa na shaka kwamba nyongeza zao hizi ilikuwa ni kosa.

Hapo ndipo Allaah (‘Azza wa Jall) akauwajibishia Ummah wa Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) kufunga mwezi huu mtukufu. Kwa sababu Allaah ameteremsha Qur-aan ndani yake. Kwa hivyo mwezi huu unatakiwa kufungwa kwa ajili ya kuishukuru neema ya Qur-aan.

---

<sup>2</sup> 02:183

## LENGO LA SWAWM NI KUMCHA ALLAAH

Allaah (Ta'ala) amesema:

لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

"... ili mpate kumcha Allaah."<sup>3</sup>

Lengo katika Aayah ni kitu ambacho ni lazima kitokee iwapo swawm itatekelezwa kwa njia ya sawa. Ni jambo lisilokuwa na shaka ya kwamba swawm ina faida nyingi ikiwa ni pamoja vilevile na:

1- Imani inapanda.

2- Uchaji Allaah unapanda.

3- Kumwogopa Allaah kunazidi.

4- Mapambano yanafanyiwa mazoezi.

5- Allaah ameifanya swawm kuwa ni sababu ya mtu kupata afya njema. Kwa ajili hiyo imekuja katika Hadiyth:

"Fungeni mtapata afya njema."<sup>4</sup>

Usahihi wa Hadiyth umetiliwa maneno.

---

<sup>3</sup> 02:183

<sup>4</sup> at-Twabaraaniy katika "al-Mu'jam al-Awsatw" (8477). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwa'iyf-ul-Jaami'" (3504).



## FUNGA NI IDADI YA MASIKU YENYE KUHESABIKA

Allaah (Ta'ala) amesema:

أَيَّامًا مَّعْدُودَاتٍ

"... [Kufunga ni] siku za kuhesabika."<sup>5</sup>

Neno أَيَّامًا ni kitendo cha pili kwa sababu ya كَتَبَ. Imesemekana vilevile kuwa ni jenitifu kwa sababu ya sentesi inayofahamika فِي أَيَّامٍ مَّعْدُودَاتٍ.

Hizi siku zenye kuhesabika ndio mwezi wa Ramadhaan. Ni siku thelathini na inaanza pale tu ambapo mwezi unapoandama.

---

<sup>5</sup> 02:184

## **KUFUNGA SIKU YA SHAKA**

Haifai kwa yeyote kufunga siku moja kabla na kwa hivyo akawa amefunga kabla ya kuyakinisha kuingia kwa mwezi mpya. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Msifunge kabla ya kuuona na msifungue kabla ya kuuona. Mkifunikwa na mawingu basi timizeni idadi ya siku thelathini."

'Ammaar bin Yaasir (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Yule atakayefunga siku ya shaka basi kwa hakika amemuasi Abul-Qaasim (Swalla Allahu 'alayhi wa sallam)."

Kwa hiyo haijuzu kufunga ile siku ya tarehe 30 Sha'baan kwa nia kwamba iwe ndio siku ya kwanza ya Ramadhāan. Kuhusiana na yule ambaye ana mazoweza ya kufunga na siku hiyo ikaangukia siku hiyo, wanachuoni wanasema kuwa hakuna neno. Hata hivyo anapaswa ajiepushe. Mtu anatakiwa kujiepusha na mambo yenye utata. Endapo atafunga siku hii kwa nia nyingine mbali na Ramadhāan na khaswa akiwa ni miongoni mwa wale ambao wanaigwa, kuna khatari wakamfuata wale wasiotambua.

## MGONJWA NA MSAFIRI KATIKA RAMADHAAN

Allaah (Ta'ala) amesema:

فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَّرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِنْ أَيَّامٍ أُخَرَ

"Yule atakayekuwa mgonjwa miongoni mwenu au safarini, basi akamilishe idadi [ya siku zilizompita] katika siku nyinginezo."<sup>6</sup>

Inajuzu kwa mgonjwa kuacha kufunga na kulipa masiku mengine. Nia yake inatakiwa iwe kulipa masiku hayo pale ambapo Allaah (‘Azza wa Jall) atapomponya.

Inajuzu vilevile kwa msafiri kuacha kufunga iwapo atanuia kuyalipa masiku yake pindi aaporejea nyumbani.

Maradhi ambayo yanaruhusu kuacha kufunga yanatofautiana. Mgonjwa ambaye ni mgonjwa sana kwa kiasi kwamba hawezi kufunga hata mara moja hatakiwi kufunga, kwa kuwa anajidhuru.

Iwapo maradhi yatakuwa mepesi kwa kiasi cha kwamba mgonjwa anaweza kufunga lakini pamoja na uzito, huyu inafaa kwake kufunga lakini hata hivyo imechukizwa. Lakini atatakiwa asifunge endapo ataonelea kuwa inamtaabisha.

Ikiwa daktari mmoja au wawili wa kiislamu watahakikisha kuwa swawm inamzidishia maradhi, itakuwa ni wajibu kwake kuacha kufunga.

Je, lililo bora kwa yule mgonjwa ambaye anaweza kufunga pamoja na kupata uzito mdogo afunge au aache kufunga? Lililo bora kwake ni yeye kufunga.

Swali hilo limeulizwa juu ya msafiri. Lililo bora kwa msafiri ni yeye kufunga au kuacha kufunga? Wanachuoni wametofautiana juu ya hili. Kuna ambao wamependekeza afunge. Wengine wamependekeza asifunge. Lakini hata hivyo tofauti hii inahusiana na pale ambapo kutakuwa hakuna tabu katika kufunga. Ikiwa kutapatikana uzito hakuna tofauti kwamba bora ni kuacha kufunga.

---

<sup>6</sup> 02:184

## UHALISIA WA SAFARI

Msafiri ni kama tulivyosema kwamba imeruhusiwa kwake kula. Ili msafiri apate ruhusa ya kuweza kuacha kufunga inatakiwa iwe ni ile safiri inayomruhusu kufupisha na kukusanya swalah. Ni jambo ambalo wanachuoni wametofautiana juu yake. Baadhi wanaonelea kuwa itakuwa inaruhusiwa ikiwa safari umbali wake ni wa siku mbili kwa kutembea na miguu. Wengine wanamaanisha kwamba ni pale ambapo safari umbali wake utakuwa wa mchana na usiku mmoja. Haya yametajwa katika upokezi kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) aliyesimulia ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Si halali kwa mwanamke anayemwamini Allaah na siku ya Mwisho kusafiri umbali wa siku tatu isipokuwa awe pamoja naye Mahram."<sup>7</sup>

Kumekuja upokezi vilevile unaotaja "mchana na usiku mmoja"<sup>8</sup>, "siku moja"<sup>9</sup> na "usiku mmoja"<sup>10</sup>. Mapokezi yote haya yametajwa na al-Bukhaariy na Muslim. Kuna upokezi uliyoko kwa Abu Daawuud unaotaja umbali sawa na takriban kilomita 20. Katika mtiririko wa wapokezi yupo mtu anayeitwa Suhayl bin Abiy Swaalih ambaye amepwekeka katika kuipokea na hali yake imetiwa dosari.

Kwa kufupisha ni kwamba tunatakiwa kuchukua ule umbali mdogo unaoitwa "safari". Safari kama hiyo ni mchana mtimilifu au usiku mtimilifu, ambao ni sawa na kilomita 40. Kwa msemu mwingine ni kwamba mtu ambaye anasafiri kilomita 40 anaruhusiwa kuacha kufunga na kufupisha swalah.

Pengine mtu akasema kuwa safari za leo zinatofautiana na safiri za wakati wa kale. Ni kweli na hii ni neema ya Allaah ('Azza wa Jall). Wakati Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipoulizwa juu ya kufupisha swalah wakati wa khofu baada ya khofu kwisha, akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

"Ni swadaqah ambayo Allaah amekupeni. Kwa hivyo ikubalini swadaqah Yake."<sup>11</sup>

---

<sup>7</sup> Ahmad (8564).

<sup>8</sup> al-Bukhaariy (1088) na Muslim (1339).

<sup>9</sup> Muslim (1339).

<sup>10</sup> Muslim (1339).

<sup>11</sup> Muslim (686).

## SWAWM YA ASIYEWEZA

Allaah (Ta'ala) amesema:

وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةً طَعَامٌ مِّسْكِينَ ۖ فَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا فَهُوَ خَيْرٌ لَّهُ ۚ وَأَنْ تَصُومُوا خَيْرٌ لَكُمْ ۖ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ

"... na kwa wale wanaoiweza lakini kwa tabu watoe fidia kulisha masikini. Na atakayejitolea kwa jema lolote lile basi ni bora kwake. Na mkifunga ni bora kwenu - mkiwa mnajua [namna ilivyo kheri kwenu]!"<sup>12</sup>

Mwanzoni ilikuwa yule anayetaka kufunga anafunga na yule anayetaka kuacha anaacha na badala yake anamlisha maskini kwa kila siku moja. Baada ya hapo Allaah (‘Azza wa Jall) akateremsha Aayah ya pili:

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ ۚ فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ

"Mwezi wa Ramadhaan ambao imeteremshwa humo Qur-aan ili iwe mwongozo kwa watu na hoja bayana za mwongozo na pambanuo la batili. Basi atakayeshuhudia miongoni mwenu mwezi mpya na afunge."<sup>13</sup>

Hapo ndipo kufunga kukawa ni wajibu kwa kila mwenye uwezo. Kwa hivyo ile hukumu ya kwanza imefutwa na kwa hivi sasa inawahusu tu wale wazee na wanawake wawazito na wanyonyeshaji ikiwa wanachelea juu ya nafsi zao au watoto wao. Inajuzu kwa mzee kuacha kufunga na badala yake akawalisha masikini. Hivyo ndivyo alivyofanya Anas bin Maalik (Radhiya Allaahu ‘anh)<sup>14</sup>.

Inajuzu vilevile kwa mwanamke mjamzito na mnyonyeshaji kuacha kufunga. Ni wajibu kwao kuyalipa masiku hayo na kuwalisha masikini au ni wajibu tu kuyalipa masiku yao au ni wajibu tu kuwalisha masikini? Wanachuoni wana maoni haya matatu. Maoni yaliyo karibu na usahihi ni kwamba ni wajibu kwao kuyalipa masiku yao pindi watapoweza kufunga. Hawahitajii kuwalisha masikini midhali hawachelei juu ya watoto wao. Hapo ndipo itakuwa ni wajibu kulisha na kuyalipa masiku yaliyowapita. Kwa kuwa walikuwa ni wenye uwezo lakini hata hivyo wakaacha kufunga kwa sababu ya kuchelea juu ya watoto wao.

---

<sup>12</sup> 02:184

<sup>13</sup> 02:185

<sup>14</sup> Maalik katika "al-Muwattwa'" (01/307).

Allaah (Ta'ala) amesema:

فَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا فَهُوَ خَيْرٌ لَهُ

"Na atakayejitolea kwa jema lolote lile basi ni bora kwake."<sup>15</sup>

Bi maana kulisha zaidi ya masikini mmoja. Hilo ni bora kwake.

Allaah (Ta'ala) amesema:

وَأَنْ تَصُومُوا خَيْرٌ لَكُمْ ۖ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ

Na mkifunga ni bora kwenu - mkiwa mnajua [namna ilivyo kheri kwenu]!"<sup>16</sup>

Allaah ameimalizia Aayah kwa kulenga ya kwamba swawm ni bora kwa wale wenye kuweza katika ile Aayah iliyofutwa.

Halafu msafiri na mgonjwa pia wanaweza kuacha kufunga wakati wa safari na maradhi. Lililo bora kwa msafiri ni kufunga au kuacha kufunga? Wanachuoni wametofautiana juu ya hilo. Baadhi wanaonelea kuwa afunge ikiwa anaweza na wengine wanaonelea aache kufunga hata kama anaweza kufunga. Hata hivyo imechukizwa ikiwa anapata uzito wa kusafiri ilihali amefunga. Ikiwa msafiri anachelea kifo juu ya nafsi yake inakuwa ni haramu kwake kufunga.

---

<sup>15</sup> 02:184

<sup>16</sup> 02:184

## QUR-AAN IMETEREMSHA KATIKA RAMADHAAN

Allaah (Ta'ala) amesema:

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ

"Mwezi wa Ramadhaan ambao imeteremsha humo Qur-aan... "<sup>17</sup>

Katika kipande hichi inapata kutubainikia kuwa Qur-aan imeteremsha katika Ramadhaan. Ni katika usiku gani iliteremka? Usiku wa Makadirio. Hili linatufanya kuamini kwa kukata kabisa ya kwamba usiku wa Makadirio uko katika Ramadhaan. Wako wanaosema kuwa usiku wa Makadirio unaweza kuwa katika Ramadhaan na nje ya Ramadhaan. Hata hivyo ni vigumu kulenga unakuwa katika usiku gani. Maoni yaliyo karibu na usawa ni kwamba unakuwa katika yale masiku kumi ya mwisho. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Utafuteni katika yale masiku kumi ya mwisho Ramadhaan na utafuteni katika kila usiku wa witiri."

Usiku wa witiri ni usiku wa tarehe 21, 23, 25, 27 na 29 Ramadhaan.

Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) ametusahilishia kwa kutujuza ya kwamba ameteremsha Qur-aan katika Ramadhaan. Katika Aayah nyingine amesema (Ta'ala):

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ

"Hakika Sisi tumeiteremsha Qur-aan katika usiku wa Makadirio."<sup>18</sup>

Hiyo haimaanishi kwamba ndipo ilipoteremka yote. Aayah hii inaweza kuwa na maana mbili:

1- Inaweza kuwa inalenga kwamba ndipo Qur-aan ilipoanza kuteremka kwa mara ya kwanza. Ilianza kuteremka katika usiku huo na ikaendelea kuteremka kwa miaka ishirini na tatu mpaka pale Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipofariki.

---

<sup>17</sup> 02:185

<sup>18</sup> 97:01

2- Inaweza kuwa inalenga kwamba ndipo ilipoteremshwa katika nyumba yenye Nguvu kwa mara moja, kama alivyosema Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa). Kisha ikawa inateremshwa hatua kwa hatua.



## QUR-AAN NDIO MAISHA YA WATU

Allaah (Ta'ala) amesema:

هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ

"... ili iwe mwongozo kwa watu na hoja bayana za mwongozo na pambanuo la batili."<sup>19</sup>

Qur-aan ni mwongozo ambao Allaah amewapa watu:

وَبَيِّنَاتٍ

"... na hoja bayana... "

Ndani yake Allaah amebainisha yaliyokuwepo na yatayokuwepo. Katu tusingelijua namna alivyombwa Adam endapo Allaah asingetujuza kuhusu hilo. Katu tusingelijua kuwa 'Arshi ya Mwingi wa huruma iko juu ya maji kabla ya kuumbwa mbingu na ardhi iwapo Allaah asingetujuza kuhusu hilo. Katu tusingelijua kuwa Nuuh ('alayhis-Salaam) ndiye alikuwa Mtume wa kwanza, kwamba aliwalingania watu wake miaka 950 na kwamba watu wake waliangamizwa kwa kuzamishwa endapo Allaah asingetujuza kuhusu hilo na mengineyo ya kale vilevile yaliyotajwa.

Vivyo hivyo inahusiana na yale yaliyoko huko mbele ya kwamba ardhi itabadilishwa, kusimama kwa Saa, ufufuliwaji, Qiyaamah, hesabu, Njia, neema za wachaji Allaah Peponi na adhabu ya Moto ya makafiri na wanafiki. Yote haya yamebainishwa na Allaah ('Azza wa Jall) katika Qur-aan hii.

---

<sup>19</sup> 02:185

## MKAZI NI LAZIMA KWAKE KUFUNGA

Allaah (Ta'ala) amesema:

فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ

"Basi atakayeshuhudia miongoni mwenu mwezi mpya na afunge."<sup>20</sup>

Hii ni amri kutoka kwa Allaah (ʿAzza wa Jall). Amri ni wajibu. Ina maana kwamba yule ambaye yuko katika mji wake pindi mwezi uandamapo basi ni wajibu kwake kufunga. Hapa ni pale ambapo atakuwa ni muweza, kishabaleghe na ni mwenye akili. Ikikosekana moja katika masharti haya basi sio wajibu kwake kufunga.

Swawm maana yake ni mtu kujiepusha na vile vinavyofunguza kuanzia pale ambapo alfajiri ya pili inapoingia mpaka pale jua linapozama kwa kunuia kufunga. Kwa msemu mwingine swawm inatakiwa kutekelezwa na mtu aliye na akili. Haiwezekani kufunga wala kufanya ʿibaadah kwa aliyekosa akili. Hapana shaka ya kwamba swawm ni faradhi na nguzo moja wapo ya Uislamu. Haya ni kwa maafikiano ya waislamu.

---

<sup>20</sup> 02:185

## WENYE UDHURU KULIPA SIKU ZILIZOWAPITA

Allaah (Tabaarak wa Ta'ala) amesema:

وَمَنْ كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِنْ أَيَّامٍ أُخَرَ

"Atakayekuwa mgonjwa au safarini basi atimize idadi katika siku nyinginezo."<sup>21</sup>

Ina maana kwamba ni wajibu kwake kulipa idadi ya zile siku alizokula pindi Ramadhan inapoisha.

Ni wajibu ulipaji iwe kwa kufululiza au sio wajibu iwe hivyo? Kuna wanachuoni wachache waliosema kuwa ni wajibu kulipa kwa kufululiza. Wanachuoni wengi wamesema kuwa sio wajibu kulipa kwa kufululiza. Wanachuoni wengi katika Maswahabah na wengineo wanaonelea kuwa sio wajibu kulipa kwa kufululiza. Dalili ya hilo ni kwamba 'Aishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) amesema:

"Nilikuwa na madeni ya siku za Ramadhan. Sikuwa naweza kuyalipa isipokuwa katika Sha'baan kwa sababu nilikuwa nikishughulishwa na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)."<sup>22</sup>

---

<sup>21</sup> 02:185

<sup>22</sup> al-Bukhaariy (1950) na Muslim (1146).

## WEPESI WA ALLAAH KWA WAJA

Allaah (Ta'ala) amesema:

يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ

"Allaah anakutakieni mepesi - na wala hakutakieni magumu."<sup>23</sup>

Aayah hii ni neema kutoka kwa Allaah juu ya Ummah wa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Mola wetu (Subhaanahu wa Ta'ala) anatumulisha kuwa anatumulikia mepesi - na wala hatutakii magumu. Kama ilivyokuja katika Aayah nyingine:

وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُم فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ

"Hakukufanyieni ugumu wowote ule katika dini."<sup>24</sup>

Makusudio ya wepesi katika Aayah ni kwamba hukumu za dini ni sahali na nyepesi. Haikusudii yale yanayosemwa na baadhi ya watu wanaposema kuwa dini ni nyepesi na huku wanakusudia kutenda kila dhambi. Watu hawa wanataka kuiwepesisha dini kwa njia hii. Watu hawa ni wenye kukosea kosa kubwa. Haki ni kwamba dini hukumu zake ni sahali na nyepesi. Kitendo cha baadhi ya watu kuthubutu juu ya madhambi na kuacha faradhi na mambo ya wajibu ya Allaah kwa madai ya kwamba "dini ni nyepesi" ni jambo lisilokuwa na uhusiano wowote ule na Uislamu.

---

<sup>23</sup> 02:185

<sup>24</sup> 22:78

## IDADI YA SIKU ZA RAMADHAAN

Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلِتُكْمِلُوا الْعِدَّةَ

"Na ili mkamilishe idadi [katika wakati wake uliyowekwa]." <sup>25</sup>

Allaah ('Azza wa Jall) anaamrisha kukamilisha idadi. Kwa ajili hiyo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Mkifunikwa na mawingu basi timizeni idadi ya siku thelathini."

Ina maana kwamba iwapo waislamu hawatoona mwezi mwandamo, basi wanachotakiwa ni wao kukamilisha Sha'baan siku thelathini. Haijuzu kufanya mwezi ukawa siku ishirini na tisa bila dalili. Lakini haina shaka kwamba mwezi unaweza kuwa siku ishirini na tisa, lakini mwezi unaofuata unaanza pale mwezi mwandamo unapoonekana. Tusipoona mwezi mwandamo basi ni lazima kukamilisha mwezi tuliopo sasa siku thelathini.

---

<sup>25</sup> 02:185

## TAKBIYR KATIKA USIKU WA 'IYD NA MCHANA WAKE

Allaah ('Azza wa Jall) amesema:

وَالْتَكْبِيرُوا لِلَّهِ عَلَىٰ مَا هَدَاكُمْ

"... na ili mumtukuze Allaah kwa kuwa amekuongozeni."<sup>26</sup>

Aayah hii ni dalili inayofahamisha kuwa ni jambo limewekwa katika Shari'ah kufanya Takbiyr katika usiku wa 'Iyd na ile siku ya 'Iyd. Wanachuoni wanatumia Aayah hii, na Hadiyth na mapokezi mengine, kuonyesha kuwa ni jambo limesuniwa kufanya Takbiyr usiku wa 'Iyd na mchana wake.

Aayah inaashiria ya kwamba Mungu wa haki na mwabudiwa ni mkubwa na mtukufu. Allaah ni mkubwa kuliko kila kitu. Allaah (Ta'ala) amesema:

قُلْ أَيُّ شَيْءٍ أَكْبَرُ شَهَادَةً ۗ قُلِ اللَّهُ

"Sema: "Ni kitu gani ushahidi wake ndio mkubwa zaidi?" Sema: "Allaah."<sup>27</sup>

---

<sup>26</sup> 02:185

<sup>27</sup> 06:19

## SWALAH YA 'IYD

Miongoni mwa Sunnah asubuhi ya siku ya 'Iyd ni kuswali swalah ya 'Iyd na kutoa Zakaat-ul-Fitwr ili kumshukuru Allaah kwa ajili ya kutimiza swawm. Allaah ameifanya siku ya 'Iyd ni siku ya furaha kwa ajili ya kukamilisha 'ibaadah ya swawm kwa njia inayopasa inayotakiwa na Allaah ('Azza wa Jall). Kwa ajili hiyo Allaah amewawekea Shari'ah waislamu watoke wende katika uwanja wa wazi na waswali swalah ya 'Iyd, wamtukuze Allaah na wamtaje ili wawe ni wenye kumshukuru Allaah ('Azza wa Jall) juu ya neema hii. Sikukuu zimewekwa katika Shari'ah kwa sababu hii.

Sikukuu nyengine zote zinazofanywa na watu hii leo ni sikukuu zilizozuliwa. Sikukuu za waislamu kwa mwaka ni mbili; 'Iyd-ul-Fitwr na 'Iyd-ul-Adhwhaa. Wana sikukuu vilevile kwa wiki, nayo ni siku ya ijumaa.

*Tuna sikukuu tatu  
kwa mwaka ni mbili; Fitwr na Adhwhaa ambayo ndio ya pili  
Ya tatu ni yenye kujirudi kwa wiki  
Hili lipo katika dini yetu tu hivyo basi jiandae*

*Hii ni fadhila ambayo Mtume wetu amefanywa kupwekeka nayo  
ni nyumati ngapi zilizotangulia zimepotoshwa kutokamana nayo!  
Zote zimefikwa kwa kumshukuru Mneemeshaji  
ambaye ameamrisha 'ibaadah kwa manufaa ya waislamu*

*Sio sikukuu zilizo na upuuzi na nyimbo  
na sio kupoteza wakati pasi na faida*

Ndio ni sikukuu, lakini zisizo na upuuzi, nyimbo na michezo. Zimewekwa kwa ajili ya kumtaja Allaah ('Azza wa Jall).

## ALLAAH YUKO KARIBU NA WAJA WAKE

Allaah (Ta'ala) amesema:

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۗ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ

"Na pindi watakapokuuliza waja Wangu kuhusu Mimi, basi Mimi ni Niko karibu; Naitikia du'aa ya muombaji anaponiomba."<sup>28</sup>

Hapa Allaah (‘Azza wa Jall) anathibitisha ukaribu Wake kwa waja Wake. Mungu mnayemuabudu yuko karibu nanyi na ni mwenye kuwatambua. Hakuna chochote katika mambo yenu kinachofichikana Naye. Ni wajibu kwenu kulitambua hilo na kumuabudu vile ipasavyo na kumuomba. Mkimuomba anakuitikieni maombi yenu akiona kuna kheri katika yale myaombao. Hapa bila ya shaka kuna maelezo juu ya kwamba Allaah yuko karibu na waja Wake, anaitikia du'aa zao na kuwahimiza nazo. Tukimuomba anaitikia. Amesema (Ta'ala):

فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ

"Basi waniitikie Mimi na waniamini Mimi ili wapate kuongoka."<sup>29</sup>

Anaitikia kwa sharti tumuitikie pale Yeye (‘Azza wa Jall) anapotuita; tusiache kufanya maamrisha Yake ambayo tunaweza kuyatekeleza au kufanya kitu cha madhambi hali ya kujua. Mtume (Swalla Allahu ‘alayhi wa sallam) amesema kuwa mja anapomuomba Allaah (‘Azza wa Jall) basi ni lazima apate moja katika mambo matatu:

- 1- Amuitikie pale (‘Azza wa Jall) atapona ni chenye kheri na yeye.
- 2- Amuepushe na shari kiwango chake.
- 3- Amuwekee maombi yake kwa ajili ya siku ya Qiyaamah.

Pindi mja anapomuomba Allaah basi anapata moja katika mambo haya matatu<sup>30</sup>.

---

<sup>28</sup> 02:186

<sup>29</sup> 02:186

<sup>30</sup> al-Bayhaqiy (3968). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Sharh al-‘Aqiydah at-Twahaawiyah" (522).



## HUTOPATA MABADILIKO KATIKA DESTURI YA ALLAAH

Allaah (Ta'ala) amesema:

فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ

"Basi waniitikie Mimi na waniamini Mimi ili wapate kuongoka."<sup>31</sup>

Hii ni dalili inayofahamisha kuwa Allaah anatuitikia tukimuitikia Yeye. Ni kama maneno ya Allaah (Ta'ala):

إِنْ تَنْصُرُوا اللَّهَ يَنْصُرْكُمْ

"Mkimnusuru [dini ya] Allaah Naye Atakunusuruni."<sup>32</sup>

Na hapa Allaah anasema:

فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ

"Basi waniitikie Mimi na waniamini Mimi ili wapate kuongoka."<sup>33</sup>

Hii ina maana kwamba endapo mja atamuitikia na kumuomba Mola wake, basi ni sababu ya yeye kuongozwa. Moja katika sababu ya uongofu ni wewe kuwa umeongozwa. Allaah (Ta'ala) amesema:

وَالَّذِينَ اهْتَدَوْا زَادَهُمْ هُدًى وَآتَاهُمْ تَقْوَاهُمْ

"... na wale walioongoka, Anawazidishia uongofu na kuuongeza uchaji wao."<sup>34</sup>

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

"Hakika Allaah hawaongozi watu mafasiki."<sup>35</sup>

---

<sup>31</sup> 02:186

<sup>32</sup> 47:07

<sup>33</sup> 02:186

<sup>34</sup> 47:17

<sup>35</sup> 63:06

Ni vipi mtenda dhambi atatarajia Allaah amwongoze ikiwa atafanya uzinzi, kunywa pombe, kula ribaa na kula mali ya haramu? Hilo ni jambo halitotokea isipokuwa ikiwa kama Allaah atamwongoza katika wema, maombi na unyenyekevu. Pindi anapomwita katika jambo la kheri, basi analikimbilia. Pindi anapomtahadharisha na jambo la shari, anajiepusha nalo. Huyu ndiye ambaye anatarajia Allaah kumwongoza.

Hata hivyo hatutakiwi kumfanya yule mtu wa pili kukata matumaini na huruma ya Allaah. Badala yake tunatakiwa kumkumbusha atubie kwa Allaah ili Allaah amsamehe, amwongoze katika yale anayoyapenda na kuyaridhia na amfanye kuyamaliza maisha yake kwa uzuri. Ama kuendelea kuyashikilia madhambi yake na machafu na kutarajia kuyapata yale watayoyapata waongofu na wachaji Allaah ni matumaini ya kipumbavu na ya batili.

## MSAMAHA WA ALLAHAH NA UKARIMU WAKE

Allaah (Tabaarak wa Ta'ala) amesema:

أَجَلٌ لَكُمْ لَيْلَةَ الصَّيِّمِ الرَّفِثُ إِلَى نِسَائِكُمْ ۖ هُنَّ لِبَاسٌ لَكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَهُنَّ ۗ عَلِمَ اللَّهُ أَنْكُمْ كُنْتُمْ تَخْتَانُونَ أَنْفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ وَعَفَا عَنْكُمْ

"Mmehalalishiwa usiku wa kufunga swawm kuwaingilia wake zenu. Wao ni vazi kwenu na nyinyi ni vazi kwao. Allaah anajua kwamba mlikuwa mkizihini nafsi zenu. Kwa hivyo amekukubalieni tawbah yenu na akakusameheni."<sup>36</sup>

Mwanzoni mwa Uislamu ilikuwa inajuzu kwa mfungaji aliyekata swawm kula, kunywa na kufanya jimaa midhali hajaswali 'Ishaa wala hajalala. Akilala au akaswali 'Ishaa basi inaharamika kwake kufanya jimaa, kula na kunywa. Halafu Allaah akataka kuonyesha huruma Yake juu ya waislamu.

Kuna mwanamume kutoka katika Answaar alikuwa akifanya kazi shambani kwake mpaka 'Ishaa. Katika wakati huo walikuwa wakibeba maji juu ya ngamia na wakiimwagilia maji mitende. Walikuwa wakifanya kazi mashambani kwa ajili ya kujipatia riziki. Alipofika nyumbani magharibi akaomba chakula. Mke wake akaenda kumtengenezea chakula. Aliporudi akamkuta amelala ambapo akamwambia kuwa chakula kimekuwa ni haramu kwake. Akaendelea na swawm yake na akaamka hali ya kuwa hana kitu tumboni. Asubuhi akaenda shambani kwake kufanya kazi na akaanguka na kupoteza fahamu wakati wa Dhuhr ambapo akabebwa kupelekwa nyumbani.

Mfano wa hayo yamemtokea 'Umar bin al-Khattwaab na waumini wengine (Radhiya Allaahu 'anhum) waliokuwa wamewaingilia wake zao. Siku moja 'Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu 'anh) alichelewa kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na akarudi nyumbani ambapo akataka kufanya jimaa na mke wake. Mke wake akamweleza kuwa amelala. Akafikiri kuwa anajipa udhuru na kuzua ambapo akamwingilia kwa kutokupenda kwake. Pindi alipomhakikishia ya kuwa kweli alilala akasikitika. Asubuhi akamwendea Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kwa kutarajia atapata makimbilio kutoka kwa Allaah kisha kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Ndipo Allaah ('Azza wa Jall) akateremsha:

أَجَلٌ لَكُمْ لَيْلَةَ الصَّيِّمِ الرَّفِثُ إِلَى نِسَائِكُمْ ۖ هُنَّ لِبَاسٌ لَكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَهُنَّ

<sup>36</sup> 02:187

"Mmehalalishiwa usiku wa kufunga swawm kuwaingilia wake zenu. Wao ni vazi kwenu na nyinyi ni vazi kwao."<sup>37</sup>

Kuwakaribia wake kunamaanishwa jimaa na ile michezo ya kabla yake. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Swawm ni kinga. Pindi mmoja wenu atapokuwa amefunga asizungumze upuuzi upuuzi (فلي يرفث) wala asigombane. Mtu akimtukana aseme: "Mimi nimefunga."

Katika maneno Yake (Ta´ala):

أَجَلٌ لَّكُمْ لَيْلَةُ الصَّيَامِ الرَّفَثُ إِلَى نِسَائِكُمْ ۖ هُنَّ لِيَاْسٍ لَّكُمْ وَأَنْتُمْ لِيَاْسٍ هُنَّ

"Mmehalalishiwa usiku wa kufunga swawm kuwaingilia wake zenu. Wao ni vazi kwenu na nyinyi ni vazi kwao."<sup>38</sup>

hapa kuna miujiza ya Allaah (´Azza wa Jall) kwa waja Wake wadhaifu na waumini.

Allaah (Ta´ala) amesema:

عَلِمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ كُفْتُمْ تَحْتَانُونَ أَنْفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ وَعَقَا عَنْكُمْ ۖ فَالآنَ بَاشِرُوهُمْ وَأَنْبَغُوا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ

"Allaah anajua kwamba mlikuwa mkizihini nafsi zenu. Kwa hivyo amekukubalieni tawbah yenu na akakusameheni. Basi sasa waingilieni na tafuteni aliyokuandikieni Allaah."<sup>39</sup>

Bi maana jimaa, kula na kunywa.

Hapana shaka kwamba hapa kuna fadhila kutoka kwa Allaah (´Azza wa Jall) juu ya waja Wake waumini kwa kule kuwasamehe madhambi yao yaliyotangulia. Kisha akawaacha wale, kunywa na kufanya jimaa katika nyusiku za funga mpaka kuingia kwa alfajiri.

---

<sup>37</sup> 02:187

<sup>38</sup> 02:187

<sup>39</sup> 02:187

## KUANZA NA KUISHA KWA SWAWM

Allaah (Ta'ala) amesema:

فَالآنَ بَاشِرُوهُمْ وَإِتَّعُوا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ ۖ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ

"Basi sasa waingilieni na tafuteni aliyokuandikieni Allaah. Kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku."<sup>40</sup>

Baadhi ya Maswahabah (Radhiya Allaahu 'anhum) walikosea katika hili na wakadhani kwamba inahusiana na maana yake ya kidhahiri ni kutazama tofauti kati ya uzi mweupe na uzi mweusi. Mtu alikuwa anaweza kufunga uzi mweupe kwenye mguu wake mmoja na uzi mweusi kwenye mguu wake mwingine halafu anakula na kunywa mpaka aone tofauti kati ya nyuzi hizo mbili. Kwani kipindi hicho hakukuwepo mataa. Anasitisha kula na kunywa pale anapona tofauti kati ya nyuzi hizo mbili. 'Adiy bin Haatim (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Ee Mtume wa Allaah! Naweka nyuzi mbili chini ya mto wangu, uzi mweupe na uzi mweusi, ili niweze kubainikiwa kati ya usiku na mchana." Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: "Basi mto wako ni mkubwa. Hilo ni giza la usiku na mwanga wa mchana." Ina maana kwamba una mto mkubwa ikiwa kama mto wako unafunika uzi mweupe na uzi mweusi ambavyo kunakusudiwa mwanga wa alfajiri na giza la usiku. Ndipo Allaah ('Azza wa Jall) akateremsha:

حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ

"... mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku."<sup>41</sup>

Nyongeza hii fupi:

مِنَ الْفَجْرِ

"... wa alfajiri... "

<sup>40</sup> 02:187

<sup>41</sup> al-Bukhaariy (4509) na Muslim (1090).

haikuteremka isipokuwa baada ya baadhi ya Maswahabah (Radhiya Allaahu ʿanhum) kuifahamu kimakosa Aayah. Kwa hivyo makusudio ya uzi mweupe ni mwanga wa alfajiri na uzi mweusi ni giza la usiku. Haya yakabainisha utatizi huu uliowakumba baadhi yao. Kisha Allaah (Taʿala) akasema:

ثُمَّ أَتُوا الصِّيَامَ إِلَى اللَّيْلِ

"Kisha timizeni swawm mpaka usiku."<sup>42</sup>

Hapa Allaah anabainisha mwisho wa swawm kama ambavyo mwanzoni alibainisha mwanzo wake. Lakini nini maana ya usiku? Ni sharti nyota zitokee, kama wanavyosema baadhi ya watu wa Bidʿah? Haya yanakwenda kinyume na maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ʿalayhi wa sallam) aliyomwambia swahabah wake mmoja pindi walipokuwa safarini:

"Teremka utuchanganyie." Akasema: "Ee Mtume wa Allaah! Bado ni mchana." Akasema: "Teremka utuchanganyie." Akasema: "Ee Mtume wa Allaah! Bado ni mchana." Akasema: "Teremka utuchanganyie. Pindi usiku utapofika hapa na mchana ukaenda kule basi amekwishakata swawm mfungaji."

Bi maana hapo itakuwa inajuzu kwake kukata swawm.

---

<sup>42</sup> 02:187

## IOGOPENI MIPAKA YA ALLAAH

Allaah (‘Azza wa Jall) amesema:

وَلَا تُبَاشِرُوهُنَّ وَأَنْتُمْ عَاكِفُونَ فِي الْمَسَاجِدِ

"Na wala msichanganyike nao hali ya kuwa nyinyi ni wenye kukaa I'tikaaf misikitini."<sup>43</sup>

Haya ni makatazo kutoka kwa Allaah (‘Azza wa Jall). Mtu anayefanya I'tikaaf haijuzu kwake kufanya jimaa na wanawake na wala haijuzu hata kubusu. Mzee aliye na matamano dhaifu inafaa kwake kubusu. Lakini mtu anayefanya I'tikaaf haifai kwake kubusu wala kukumbatia katika hali yoyote. Haya ni haramu. Allaah (Ta'ala) amesema:

تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ

"Hiyo ni mipaka ya Allaah."<sup>44</sup>

Kitendo hichi ni katika mipaka ya Allaah. Yule mwenye kuchanganyika na mwanamke iliali ni mwenye kufanya I'tikaaf amevuka mpaka wa Allaah. Allaah (Ta'ala) amesema:

تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَقْرُبُوهَا

"Hiyo ni mipaka ya Allaah, hivyo basi msikaribie."<sup>45</sup>

Hii ni dalili inayofahamisha kuwa ni haramu kuchanganyika na wanawake wakati wa I'tikaaf na ni moja katika mipaka ya Allaah aliyoiharamisha.

---

<sup>43</sup> 02:187

<sup>44</sup> 02:187

<sup>45</sup> 02:187

## KUIADHIMISHA MIPAKA YA ALLAAH NI KATIKA 'IBAADAH KUBWA

Allaah (Ta'ala) amesema:

كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ آيَاتِهِ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

"Hivyo ndivyo Allaah anavyobainisha Aayah Zake kwa watu ili wapate kumcha."<sup>46</sup>

Bi maana kama ambavyo Allaah amekubainishieni vilevile mipaka ya swawm na ya mambo mengine. Katika baadhi ya Aayah kumbainishwa shari ili iepukwe na Aayah zengine zimebainisha yenye kuruhusiwa ili watu waweze kuyatekeleza. Ni wajibu kwetu kusimama katika mipaka ya Allaah. Yale ambayo Allaah ameturuhusu hakuna ubaya kuyafanya. Yale ambayo ametukataza ni wajibu kwetu kuyaepuka na kuyaogopa. Ni juu yetu kutekeleza faradhi za Allaah kama alivyotaka Allaah na wajibu kwetu kujiepusha na makatazo ya Allaah, ili Allaah awe radhi na sisi na tuwe ni wenye kumshukuru Allaah ('Azza wa Jall).

Mwisho

---

<sup>46</sup> 02:187